# CHUSOMENI

# KIBAJUNI

# KIVANGO 3

Yumna Hamid Titi

Fuad Aroi

Yumbe Athman

TWAWEZA COMMUNICATIONS
Working Towards a Better World

Shungwaya Welfare Association
Umoja ni Nguvu

SWAHILI RESOURCE CENTRE
Old Town, Sir Mbarak Hinawy Road
Mombasa

Kimechapishwa na:

Twaweza Communications Ltd.
Jumba la Twaweza, Barabara ya Muthithi
Mpesi Lane
S.L.P. 66872 - 00800 Nairobi, Kenya
Simu: +(254) 020 269 4409; 0727 427740
Barua pepe: info@twawezacommunications.org
Wavuti: www.twawezacommunications.org

©Haki a kunakili nḏa Twaweza Communications
Chapisho la Kwanḏa 2024

**ISBN: 978-9966-128-18-8**

Kiṯabu cha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a nradi wa kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Nradi huu huṯekeledhwa na kichuo cha Twaweza Communications, Shungwaya Welfare Associaṯion na Swahili Resource Centre. Undofadhiliwa na nfuko wa British Council Protection Fund kwa ushirikiano na UK's Department for Culture, Media and Sport.

BRITISH COUNCIL
In partnership with
Department for Culture, Media & Sport
Cultural Protection Fund

Approved by KICD

# Aliomo

1: Kuivisha Iye Na Vangine . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

2: Jamii. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5

3: Vaṉama Va Mwichuni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 10

4: Usalama Barabarani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16

5: Misimu Mbalimbali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 21

Approved by KICD

# SHUKURANI

Dhiṯabu dha *Chusomeni Kibajuni* ni sehemu a juhudi a kulindra na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni. Chwaṯoa shukurani kwa mfuko wa British Council Protection Fund kwa nsaada ulochuwedhesha kuanḏika na kuchapisha dhiṯabu hidhi. Bila nsaada wavo ingalikuva ṯabu sana kuvapa vana va Kibajuni nafasi a kuifundrisha kusoma na kuanḏika Kibajuni. Chwavashukuru Dkt. Rukiya Harith na Nafisa Awadh kwa ushirikiano wavo na vaanḏishi kachika haṯua dhoṯe dha kuanḏika nfululuḻidho wa *Chusomeni Kibajuni*. Vaandishi va dhiṯabu hidhi – Yumna, Aroi na Yumbe – valiiṯolea kushiriki na kumalidha kuanḏika. Chwavashukuru sana kwa nchango huu muhimu. Pia chwanshukuru Athman Tora (Lalavani) na vale voṯe chufanyao navo kadhi hii adwimu a kuhifadhi na kuimarisha uṯamaduni wa Vabajuni.

Kimani Njogu, Twaweza Communications
Omar Lali, Shungwaya Welfare Association
Athman Lali Omar, Swahili Resource Centre

Juni, 2024


Approved by KICD

# 1 KUIVISHA IYE NA VANGINE

## Kusikidha

Sikidha anenwao kwen̲e chepu

### Maagidho

Vanafund̲i vakiva na mwalimu wavo vasikidhe chepu darasani.

### Jibu masuali

1. Chaya baadhi a maneno uliosikia ..........................................
2. Chaya mambo vaambianao......................................................
3. Havo vadhungumudhao ni mbani?............................................
4. Vadhungumudhao vako kachika hali gani?................................
5. Ni madhuri api alioko kachika uneni wavo?................................




Approved by KICD

## Kudhungumudha

### Madhungumudho

Juta: Mwenechu Yadhi, mbona yana hukumalidha kadhi dha ṉumbani chwalopawa na mwalimu?

Yadhi: Sina la kukuhadisia abawa Juta. Yana nalikuva nchovu wa nvili, mikono ilikinuṯura kama kiṯesi.



Juta: Hunishindi imi, yana niliṉoka mwakisuni kama fiha.

Yadhi: Alikuvae mambo hao? Ṯena hukuvona maṯo ako afurie kwa usinḏidhi.

Juta: Oṯe haa nikuṯulubu radhi dha vadhee, manake nalidhingilia nguvo dhavo kadhifua na kudhiova kwa sabuni mpaka dhikachakacha.

Yadhi: Ndroo uwe walifanya yambo la uchu lalonifanya nami kuṯeka mpaka menyo akakosa kuuma nkache.

Juta: Hela nambia nami, uwe kiva hukumalidha kadhi dha sukuli huvae?

Yadhi: Imi kiva siyafanya kadhi dha sukuli huva muwee, nikava sina raha na dhikava hunifa ganḏi.

Juta: Masikini! Hukuombea Mungu uwedhe kumalidha kadhi dhako kwa majira afaao.


Yadhi: Amina Rabbilalamina.

### Maagidho

Mwalimu avavulidhe vanafunḏi masuali kuṯokana na madhungumudho hao.

# Kusoma

## Kusoma Senchensi




Imi ni mwanafunḏi wa kivango cha chachu. Huifundra kusoma kwa juhuḏi dhangu dhoṯe.




Imi ni asikari nipenḏao uchulivu na amani.




Kwa urefu wa kimo na rahi dha nvili, naliwedha kufunga magoli maaṉe kwa kuḏangua mpwira kwa kiṯwa.



Approved by KICD

## Kuanḏika

### Kuundra Senchensi

### Masuali

**Undra senchensi kwa kulinganisha maneno mahalipe**

1. Kiṯwa hunifuka mocho changu.

   ……………………………………………………………

2. ndrani hunifungia kidha maṯo.

   ……………………………………………………………

3. nisirevee niṯafanya ṉima biḏii.

   ……………………………………………………………

4. Iko mbali n'yini sukuli na

   ……………………………………………………………….

## Kuanḏika

### Kukamilisha Senchensi

### Masuali

Ṯaua maneno kuṯoka kweṉe kikapu cha mwalimu kisha uayadhe kweṉe senchensi

1. Ina langu ni ………………………..
2. Imi niko ………………… cha chachu
3. Mayonḏi …………………..
4. Naliposikilia nchoni nalibika ……………………
5. Ukinipa wisha na bakae niṯapokea ……………………..
6. Uwe ni …………………… angu.

Approved by KICD

# 2 JAMII

## Kusikidha

Sikidha nganu a mwalimu



### Maagidho

**Sikidha nganu a mwalimu kisha ujibu masuali**

1. Ni maneno gani ambao amechaywa na mwalimu ahusianao na kadhi? ........................................................................
2. Ni kadhi gani ikuchuao?..................................................
3. Ukulima ni kadhi gani?....................................................
4. Udakiṯari ni kadhi gani?....................................................
5. Chaya mashuhuli uaivao kachika jamii..............................



Approved by KICD


## Kadhi a n̲umbani

Kat̲afudhe  nganu fupi kut̲oka kwen̲e kifaa cha kidigichali kama simu ukisaidiwa na jamaa va n̲umbani.

# Kudhungumudha

## Kadhi Mbalimbali

Vachae hava ni mbani na hufanya shuhuli gani?




## Maagidho

Vanafun̲di vaeledhe ni kadhi gani dhilidhoko kwen̲e picha.

## Kusoma

### Ufahamu

**Kadhi dha jamii**







Ama dhamani dha kale na dha sasa hadhifanani hasa kachika shuhuli dha jamii.

Chukienga upande wa mahadhigi vadhamani, havakuchumia sindano bali valikichokosa ḏawa kunwa na kuisania nvilini.Valikilima vakichumia majembe, dhisalima na dhiṯoka badala a kulima kwa gari la kukokocha. Vaṯonyi va eo huchumia mabochi makuru badala a majahadhi, maema na mundru kachika kuovea isi.

Kadhi dha siku hidhi ni pesa sana si kama za kae, uṯavavona rubani, valimu na asikari voṯe ni nyange na havachomoki kwa sababu valisoma dhikasomeka valipokuva sukuli.

Vale vafuao dhuma pamoya na vachuudhi va biashara ndrodi ndrodi vana bidii kachika kuṯafudha ridhiki dha halali.

Hakika kachika jamii muna mashuhuli mbalimbali a kuipachia mapacho.



Approved by KICD

### Jibu masuali

1. Hadhigi hufanya kadhi gani kachika jamii?

   ....................................................................................

2. Nkulima wa dhamani alikuva akichumia dhifaa gani?

   ....................................................................................

3. Rubani na valimu valifanyae mpaka vakaipacha kadhi hio?

   ....................................................................................

4. Faida gani aipachao nchu afanyao kadhi?

   ....................................................................................

5. Vaṯonyi va eo huchumia nini kuṯomea?

   ....................................................................................

## Kuanḏika

### Kuundra harufu

**Maagidho**

Ṯaba harufu hidhi kweṉe kiṯabu kisha udhisinage kwa vuongo

| |
|---|
| Aa Bb Cc Dd Ee Ff Gg Hh Ii Jj.................. |

### Kadhi a dhiaḏa

Anḏika maneno usemewao na mwalimu

1.
2.
3.
4.

## Kuanḏika

### Haṯi

### Maagidho

**Anḏika senchensi hidhi kwa udhuri**

1. Ukulima ni kadhi nḏuri.
2. Kadhi huecha mapacho n'yini.
3. Uyudhi ni muhimu maishani.
4. Mai akifuma, chombo hupwewa.
5. Avu ni faṯini wa kuchora.

### Andika nchungo kuhusiana na picha hiyo



Ieledhe kadhi hii kwa kuanḏika senchesi ṯano

1.
2.
3.
4.





Approved by KICD


# 3 VAṈAMA VA MWICHUNI

## Kusikidha

### Dhilio dha vaṉama va mwichuni







### Maagidho


a. Mwalimu avasikidhishe vanafunḏi sauṯi mbalimbali dha vaṉama na kuvavonesha vidio.

b. Vanafunḏi vaṯabe sauṯi mbalimbali dha vaṉama va mwichuni.

Approved by KICD

## Kudhungumudha

### Umuhimu wa vaṉama va mwichuni



**Kadhi a dhikundri**

Vanafunḏi vadhungumudhe kuhusu umuhimu wa vaṉama va mwichuni.

## Kudhungumudha

### Kulindra vaṉama va mwichuni

#### Maagidho

Kachika dhikundri dhungumudhani kuhusu sampuli mbalimbali dha kulindra vaṉama va mwichuni.

**Nfano:**

a) Vasivinḏwe.

b) Vasiharibiwe makaadhi avo.



Approved by KICD

# Kusoma

## Kusoma



## Hifadhi dha vaṉama va mwichuni

**Soma madhungumudho haa kisha ujibu masuali**

| | |
|---|---|
| Mwalimu: | Huyambo asikari? |
| Asikari: | Siyambo mwalimu, karibu kachika makaadhi a vaṉama. |
| Mwalimu: | Asanṯa. |
| Asikari: | Mevona nḏovaecha vanafunḏi vavone vaṉama va mwichuni. |
| Mwalimu: | Nkweli asikari. |
| Asikari: | Hamuyambo vanafunḏi karibuni kachika hifadhi a vaṉama. |
| Vanafundi: | Hachuyambo, chumefurahi kuya hapa. |

Approved by KICD

| | |
|---|---|
| Asikai: | Mwapend̲a kuvona van̲ama gani? |
| Mwanfundi 1: | Napend̲a kunvona simba. |
| Mwanafundi 2: | Imi nat̲aka kunvona nachi. |
| Asikari: | Ehhee! Hapa mut̲avona van̲ama vot̲e va mwichuni. |
| Mwanafundi 3: | Nami nat̲aka kunvona t̲uvi na pisi. |
| Asikari: | Bila wasiwasi mut̲avavona van̲ama vot̲e. |
| Mwanafundi 1: | Nina suali,"Mbona hava van̲ama vafund̲iwa na kulindrwa?" |
| Asikari: | Hii ni nd̲ia moya a kuvalindra ili vasivuwawe na majangili. |
| Mwanafundi 4: | Mbona huvuwawa van̲ama hava? |
| Asikari: | Kuna sababu n̲ingi dha kuvuwawa kama: kwa ajili a n̲ama, ngodhi, pembe, menyo na madowe. Pia kuna vachu vangine huvavuwa ili kuilindra ivo veneve na hondre dhavo dhisiharibiwe. |
| Mwanafundi 5: | Kuna sababu ngine? |
| Asikari: | Ndio, van̲ama mwichu hupendedha vat̲alii na nchi echu hupacha sint̲i n̲ingi dha kigeni. |
| Mwanafundi 2: | Hae chupeke chuvavone havo van̲ama. |
| Asikari: | Chwendreni, ivani makini na muand̲ike maina a van̲ama vot̲e muvavonavo. |

## Jibu masuali

1. Vanafund̲i vamekwendra kwapi?............................................
2. Ni van̲ama gani valochaywa kachika madhungumudho haa?.............
   ....,...................,...................
3. Mwanafund̲i wa kwand̲a alipend̲a kumvona nnyama upi?.................
4. And̲ika sababu mbili dha kuvalindra van̲ama mwichu ...........................
   .........., ............................................
5. Vavuao van̲ama mwichu huichwae?...................................



Approved by KICD

# Kuanḏika

## Kuundra senchensi

### Maagidho

Apange maneno haa kuundra senchensi sawa

a. mfalume ni simba mwichuni wa

b. sana mbio ana ṯuvi

c. alivamia muyi simba

d. ndrefu chiga una koo

## Kadhi a dhiaḏa

Chunga senchensi ukichumia maneno haa

a. Jangili

b. Mwichuni

c. Nachi

d. Vaṯalii

# Kuanḏika

## Kuchunga senchensi

### Maagidho

Chunga senchensi ṯanu kuhusu ulindraji wa vaṉama va mwichuni.

## Kadhi a dhiad̠a

### Nraba

T̠afudha maina a van̠ama va mwichuni

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| N | S | H | K | M | P |
| Y | I | T̠ | U | V | I |
| I | M | J | L | U | S |
| H | B | M | V | T̠ | I |
| C | A | O | W | Y | V |
| A | D | R | X | O | M |
| N | A | C | H | I | A |




Approved by KICD

# 4 USALAMA BARABARANI

## Kusikidha

### Hadisi



### Maagidho

Kwa dhikundri vanafunḏi vaṯoleane dhisa kuhusu ajali dha barabarani.

Approved by KICD

## Kudhungumudha

### Shairi

**Soma shairi hili kwa sauṯi**

Huvaeledha ndrudhangu, maneno eṉe mashiko,
Usalama ni wa Mungu, lakini hadhari iko,
Chunga huumwi na ṯungu, nchocho shauri ako,
Usalama barabarani, chuuṯunḏeni muhimu.

Sharia dha chirafiki, ni muhimu dhianḏamwe
Nvukaji huna dhiki, na husumbuliwi kamwe,
Kiyani kiviṯi ikiafiki, ṯaa a nehundru idhimwe,
Usalama barabarani, chuuṯunḏeni muhimu.

Pindri ikivaka redi, ḏereva komesha gari,
Yelo ikiṯaraḏaḏi, ḏereva keṯi ṯayari,
Kijani ndrio ahaḏi,nendra sasa ni shuari,
Usalama barabarani, chuuṯunḏeni muhimu.


Kuna dhebura kurosi, rangi a pundra milia,
Usiendreshe kwa kasi, gari lako pungudhia,
Ṯasababisha mikosi, kishaa ukiichia,
Usalama barabarani, chuuṯunḏeni muhimu.



Approved by KICD

## Kusoma

### Ufahamu



## Sharia Dha Barabarani.

Ni ladhima kwa kila nchu kuṯukuwa ṯahadhari na kuva mwangalifu avukapo barabara. Waṯakiwa kuva makini, kwani barabara si sehemu a kuṯedhewa. Uvukapo barabara waṯakiwa kuangalia pandre dhoṯe mbili, kulia na kusoṯo ili kuhakikisha hakuna gari.

Sharia dha barabarani huchuekedha sehemu salama ambadho wawedha kuvuka, kwa nfano kuchumia daraja la kuvukia, kuvuka kweṉe alama dha pundra milia na kuangalia michoro a ṯahadhari.

Maḏereva vaṯakiwa vave vaangalifu sana. Ajali ṉingi husababishwa na maḏereva ambavo havako makini. Serikali yaṯakiwa kuvaṯukulia haṯua kali ḏereva yoyoṯe aṯakaovunḏa sharia. Ni ladhima kwa kila ḏereva ave na leseni.

Magari maovu asikubaliwe kamwe kuchumika. Ni jukumu lechu isi kuwedha kunkomesha ḏereva aendreshao gari kwa mwendro wa kasi sana. Ivapo chuṯanyamaa, hwendra akasababisha ajali mbovu nno vachu vakapoṯedha maisha avo. Isi voṯe chuveni makini na vaangalifu. Barabara mbovu dhirekebishwe ili kupungudha dhifo dhiṯokeadho kila siku, chembelecho ajali haijali.

## Masuali

1. Uvukapo barabara waṯakiwa uve _________.
2. Uvukapo barabara waṯakiwa kuangaliya pandre gani? _________ na _________
3. Ni sehemu gani salama dha kuvukia barabara? _________
4. Ni ladhima kila ḏereva ave na _________
5. Magari _________ asikubaliwe kuchumika.


Approved by KICD

# Kusoma

## Kusoma senchesi

**Mukiva vavili vavili somani senchensi hidhi.**

1. Usivuke mbee a magari a dharura.
2. Ḏereva nlevi alisababisha ajali.
3. Magari maovu aondrolewe barabarani.
4. Darajani ni sehemu salama a kuvukia.
5. Usivuke kachikachi a magari aloegeswa.
6. Funga nshipi ukiva garini.
7. Vuka sehemu salama.
8. Dhifo dhingi husababishwa na ajali.
9. Usikimbie barabarani.
10. Usiṯedhe kachikachi a barabara.

# Kuanḏika

**Anḏika senchesi ukiṯumia maneno haa.**

1. Kidhibiṯi mwendro
2. Ajali
3. Barabara
4. Ḏereva
5. Asikari

# Kuanḏika


## Kuanḏika nchungo

**Anḏika nchungo nfupi kuhusu usalama barabarani.**

# 5 MISIMU MBALIMBALI

## Kusikidha

### Misimu mbalimbali




### Maagidho

Kachika dhikundri jadilianani kuhusu misimu mbalimbali kulingana na michoro.



Approved by KICD

## Kudhungumudha


### Njaḏala

Nsimu wa vua ni bora kuliko wa yuva.

## Kusoma

### Ufahamu

**Misimu mbalimbali**



Nsimu ni kipindri kachika mwaka ambapo hali maalumu a hewa hupachikana. Mabadiliko a hali a hewa kachika kipindri fulani cha mwaka hudhihirisha misimu mbalimbali. Misimu huirudia rudia kila mwaka. Kuna nsimu wa yuva ikali, nsimu huu mara ṉingi huva na **chaka** na upepo nkali, huichwa **kasikadhi**. Mimea na vaṉama hudhoofika sana kwa kukosa mai na chakula.

Nsimu nngine ni nsimu wa vua ṉingi, huu huichwa kusi.Vua ikidhiḏi nao husababisha dhimba.Vakulima hufurahia vua lakini isive a kupicha kiasi. Nsimu nngine ni nsimu wa **dhoruba**. Hapa upepo nkali huvonekana. Dhombo baharini hudhama.Vaṯonyi hukosa kwendra kuṯoma kwa kuhofia maisha avo na hasara a majahadhi kudhama.

Kuna nsimu nngine wa vua dha **rasha rasha**. Nsimu huu pia huva na baridi. Vua hii pia huichwa vua a kilimo. Dhichakwi hupachikanwa kwa wingi, vua hii ndio husaidia mimea kuchengedha dhakula. Kuna wakaṯi nngine ambapo huva na upepo uvumao kuṯoka **kusi** na **maṯilahi** na vanavosafirisha dhombo baharini huṯegemea pepo hidhi.

**Jibu masuali**

1. Eledha maana a nsimu.................................................................
2. Chaya aina a misimu kachika mwaka..........................................
3. Ni nsimu gani vaṯonyi hushindrwa kwendra baharini?....................
4. Vakulima hufurahia nsimu upi?......................................................
5. Mariamu wenḏee sukuli uvadhie suecha. Wafikiri huu ulikuwa ni nsimu gani? ....................................................................

## Kusoma

### Kusoma senchesi

1. Kachika mwaka kuna misimu mbalimbali.
2. Vua ṉingi hunya nsimu wa kusi.
3. Upepo wa maṯilahi ni ndhuri kusafirisha chombo.
4. Vua ikinya ṉingi husababisha dhimba.
5. Wakaṯi wa yuva ikali michi hukauka.
6. Upepo ukiva mwingi usendre baharini.



Approved by KICD

## Kuanḏika

### Nraba

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | I | A | N | G | A | D | H | I |
| B | S | M | K | C | K | H | D | L |
| C | K | L | U | H | G | O | S | R |
| R | D | K | S | A | Y | R | W | A |
| H | E | W | I | K | F | U | Ṯ | H |
| M | A | Ṯ | L | A | I | B | N | D |
| V | R | O | J | U | V | A | J | V |

### Maagidho

Chumia nraba kujibu maswali afuachao..

1. Nsimu wa vua ṉingi ni ______________
2. Ni nsimu gani mimea hukauka? ______________
3. Wakaṯi wa kiangadhi huva na nini? ______________
4. Ni nsimu gani vaṯonyi hushindrwa kwendra kuṯoma?

   ______________
5. Upepo gani manahudha hupenḏa kusafiria? ______________

## Kuanḏika

### Kuanḏika nchungo

### Maagidho

Anḏika nchungo kuhusu shuhuli mbalimbali dhifanyikadho wakaṯi wa misimu mbalimbali a mwaka.